# Learning by Ear – Climate Change

## Episode 03

**Text: Victoria Averill**

**Editing: Johannes Beck**

**Kisuaheli: Eric Ponda**

CHARACTERS:

Scene 1:

- JOSHUA (15)
- MR BENSON – JOSHUA'S FATHER (40)

Scene 2:

- JOSHUA (15)
- LORNA (16)
- MRS KIMAU – SCIENCE TEACHER & LORNA'S MOTHER (45)
- CAROL (14)

Scene 3:

- JOSHUA (15)
- LORNA (16)
- CAROL (14)

- ALEX (15)

**Intro:**

Karibu msikilizaji kwa makala ya tatu ya mchezo wa Radio "Noa Bongo Jenga Maisha yako" tukiwa bado tunazungumzia suala la mabadiliko ya hali ya hewa.

Mambo yanazidi kupamba moto na iwapo wanafunzi hawatachukua hatua za haraka kupinga ujenzi wa kiwanda cha umeme cha Dhowville, huenda mradi huu utaendelea kama ilivyopangwa. Lakini Josh anaona maisha ya Babake yakizidi kuathirika kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa na sasa anajitolea kumsaidia. Je kundi hili la wanafunzi litafanikiwa, na ni wapi litaanzia ?

Uendelea kuwa nasi hadi mwisho wa kipindi ili ufahamu jinsi mambo yanavyokwenda.

## Scene One: on the beach by the sea

**SFX ATMO:** **STORMY SEAS, THUNDER**

**1. JOSHUA:** **(shouting)** Habari Baba, nimekuja kukusaidia kuvuta dau hadi ufuoni. Nirushie kamba hiyo!

**2. MR BENSON:** **(shouting above sound of waves)** Asante sana Josh, Fanya upesi si unaona mawimbi yanavyozidi kuongezeka. Unayaona…!

**3. JOSHUA:** Ndiyo, niko tayari!.

**SFX:** **THUD OF ROPE IN THE WATER**

Nimeipata! Acha nikuvute sasa!

**(lots of grunting and groaning as the boat is heaved onto the shore)**

**4. MR BENSON:** **(sigh)** Usiku ulikuwa mgumu na tazama licha ya juhudi zote za usiku kucha hakuna chochote tunachoweza kudhihirisha kukaa kwetu baharini muda wote huo wa masaa 12…! Na hali hii ya hewa imetoka wapi? Kawaida hatupati dhoruba wakati huu wa mwaka!

**5. JOSHUA:** Baba hapa huwa hakuna samaki wengi, kwanini?

**6. MR BENSON:** Sina uhakika Josh!.Nimevua samaki mahala hapa kwa muda wa miaka kumi lakini….siku hizi hakuna tena samaki. Yaonekana wanahamia mbali kwenye kina baharini, na mimi siwezi kwenda kuvua huko peke yangu!.

**7. JOSHUA:** Samaki wanahamia kwenye kina cha bahari. Kwa nini?

**8. MR BENSON:** Natamani ningejua! Wale jamaa kwenye soko la samaki wanazungumzia ongezeko la ujoto duniani na kupanda kwa kiwango cha joto baharini. Natamani ningefahamu mengi zaidi kuhusu suala hili lakini mimi sikusoma. Ninachofahamu ni kwamba kuna kitu kinachokwenda kombo baharini,na kwa samaki.

**9. JOSHUA:** Lakini mbona Samaki bado wanapatikana kwa wingi sokoni?

**10. MR BENSON:** Nadhani hao wanatoka kwa wavuvi wanaotumia vikokoozi. Wavuvi hawa huwa na vifaa madhubuti vinavyoweza kuvua samaki maili nyingi kutoka ufuoni. Lakini Josh lazima niseme nina wasi wasi kidogo.

**11. JOSHUA:** Mmm.

**12. MR BENSON:** Lakini ni sawa tu…! Hebu tufanye haraka kuondoa hizi nyavu na Samaki wetu kabla dhoruba kutufikia, na kisha unajua lazima uende shuleni!

**SFX:** **BOXES BEING CLOSED**

**SFX:** **STORM BUILDING UP**

## Scene Two: in the street, then inside a driving car

**SFX ATMO:** **RAIN, CARS DRIVING PAST IN RAIN GOING THROUGH PUDDLES**

**13. JOSHUA:** **(to himself)** Nachukia sana kutembea kwenda shuleni kukiwa hivi! Kama tungekuwa na pesa za nauli ya basi au hata motokaa!

**SFX:** **CAR DRIVING PAST AND SPLASHING THEN STOPPING**

**14. JOSHUA:** Oh Mungu wangu! Kama tu nilivyokuwa nikiomba. Nimelowa chepechepe!

**15. LORNA:** Habari Josh ,ni mimi Lorna. Ingia ndani nitakupa lifti hadi shuleni.

**16. JOSHUA:** **(running, breathless)** Asante sana Lorna, Asante Bibi Kimau!. Kweli nimelowa chepe!

**SFX:** **OPENING, CAR DOOR, CLOSING DOOR**

| | |
|---|---|
| **SFX ATMO:** | **DRIVING INSIDE CAR, WINDSCREEN WIPERS** |
| **17. MRS KIMAU:** | Leo umerauka kwenda shule, Josh! |
| **18. JOSHUA:** | Aah kwa kweli nilikuwa nikimsaidia babangu kuvuta dau lake ufuoni na kupakua samaki. Lakini sio eti walikuwa samaki wengi viiiile!. |
| **19. LORNA:** | Kwa nini? |
| **20. JOSHUA:** | Katika miaka michache iliyopita amekuwa akivua samaki  wachache sana, na wanazidi kupungua..! |
| **21. MRS KIMAU:** | Hiyo inaonekana kuwa athari nyengine ya mabadliko ya hali ya hewa Josh! Kiwango cha joto baharini kinazidi kuongezeka. Na hali inazidi kuwa ngumu sana kwa wavuvi kama Babako. |

**22. JOSHUA:** Lakini kuongezeka kwa kiwango cha joto baharini kunasababisha vipi kuwa na samaki wachache baharini?

**23. MRS KIMAU:** Mikondo ya maji baridi huleta chakula kingi cha samaki na hivyo kuwawezesha kuzaana kwa wingi. Kwa hivyo kiwango cha joto kinapopanda baharini, samaki huhamia sehemu za kina baharini kutafuta sehemu zenye ubaridi mbali kabisa na ufuoni.

**24. JOSUA:** Ahh, kumbe! Na Babangu hawezi kufika mbali hivyo.

**25. MRS KIMAU:** Nao wataalam na wanasayansi wanasema hali hii imesababishwa na El Nino .

**26. LORNA:** Nimesikia kuhusu El Niño. Kwani watu hawajui kwamba El Niño inachangia kwa kiwango fulani mabadiliko ya hali ya hewa tunayoshuhudia kwa hivi sasa na ambayo yanaharibu matumbawe yetu ufoni?

| | |
|---|---|
| **27. MRS KIMAU:** | Ni kweli. Kwa ufupi El Niño ni mabadiliko ya mikondo ya maji kutoka hali ya ubaridi hadi joto katika bahari ya Amerika Kusini. Hali hii hutokea kwa kipindi kifupi kila mwaka, lakini mara nyingine mikondo ya joto hudumu kwa kipindi kirefu na husababisha mabadiliko ya hali ya hewa kote kote ulimwenguni. |
| **28. LORNA:** | Na mabadiliko hayo ndiyo yanayofahamika kama El Niño, sivyo? |
| **29. MRS KIMAU:** | Hasa! Si unaona athari zake hapa Dhowville, ambapo kiwango cha joto baharini kimeua matumbawe yote. Sababu nyingine ya kupotea kwa Samaki, ni kwamba maeneo yao ya kuzaana yameharibiwa. |
| **30. LORNA:** | Na pia ni lazima tujipongeze kwa juhudi zetu katika kuchangia uchafuzi wa mazingira. Ni jambo la kuudhi sana hasa nikifikia mradi wa ujenzi wa kiwanda kipya cha Umeme. |

**31. MRS KIMAU:** Ni kweli, lakini unajua yapo masuala mengine yanayochangia mabadiliko ya hali ya hewa.

**32. JOSHUA:** Kwa mfano magari tunayotumia kwa hivi sasa! Na vipi kuhusu ndege zinazowasafirisha watalii kuja hapa kwetu kupumzika ufuoni? Hutumia mafuta mengi na pengine kutoa viwango vikubwa vya gesi zinazoharibu mazingira.

**33. MRS KIMAU:** Ndege huenda zikawa watoaji wakubwa wa gesi inayochafua mazingira. Pamoja na kutoa dioksidi ya kaboni  wakati zinapochoma mafuta pia hutoa ain mbili ya gesi za oksaidi ya naitrojeni na mvuke. Na kwa kuwa hupaa juu kabisa karibu au katika eneo la anga juu ya hewa ya kawaida, wanasayansi wanasema husababisha uharibifu zaidi.

**34. JOSHUA:** Ni makosa. Hebu mtazame babangu. Hajatia guu lake kwenye ndege, hana gari ni ani nadra kutumia basi. Lakini yeye ndiye anayeteseka kutokana na ongezeko la ujoto na tabia ya watu wengine kutowajibika.

**35. MRS KIMAU:** Ni kweli Josh. Hiyo ndio sababu sisi hapa barani Afrika ndio tunaoathirika zaidi na mabadiliko haya ya hali ya hewa.Lakini hata hivyo tuna nafasi nzuri ya kunufaika zaidi iwapo tutaimarisha juhudi za kuhifadhi mazingira yetu.

**36. LORNA:** Tunahitaji kuanzisha  jopo litakaloshughulikia masuala haya bila kuchelewa.

**37. JOSHUA:** Jopo la kushugulikia athari zinazotokana na mabadiliko ya hali ya hewa? Nimelipenda wazo hilo!

| | |
|---|---|
| **38. MRS KIMAU:** | Nitakupatia nambari za simu za watu unaoweza kwenda na kuzungumza nao. Na ni vyema uanze na mwanasayansi wa maswala ya mazingira. |
| **39. JOSHUA:** | Tukutane wakati wa chakula cha mchana kulijadili kwa kirefu zaidi suala hili. Ah, hebu mtazame! Carol yelee tayari yuko uwanjani! |
| **SFX:** | **CAR ENGINE TURNING OFF, DOORS OPENING** |
| **SFX ATMO:** | **PLAYGROUND SOUNDS** |
| **40. CAROL:** | Habari zenu? Hebu tazameni nilivyorowa. Kila mahali kumefurika. Unaweza kuamini mvua hii ya mwezi huu wa Januari? |

**Scene Three: School canteen**

| | |
|---|---|
| **SFX ATMO:** | **CANTEEN – STUDENTS EATING** |
| **41. LORNA:** | Ehhe Carol, Alex, mko tayari kwa jopo hili? Je, mnataka kuendelea na juhudi zenu za kupinga ujenzi wa kiwanda hiki cha umeme? |

**42. CAROL:** Bila shaka mimi niko mstari wa mbele. Nimechoshwa kabisa kuona kampuni zikiendelea na tabia hii.

**43. LORNA:** Vyema ! Alex?

**44. ALEX:** Sijui. Yaani nina maana kufikia mwishoni mwa wiki iliyopita sikuwa naamini chochote kuhusu swala hili la mabadiliko ya hali ya hewa. Na ingawa najionea mwenyewe kinachoendelea katika mazingira yetu, na nadhani ni kweli, itakuwa na maana ya kupiga vita dhidi babangu na hiyo itakuwa vigumu.

**45. JOSHUA:** Huo ni mtanziko Alex, kwa sababu iwapo babako na washirika wake wataendelea na mradi huu, atafaidika kifedha ndio, lakini hebu mtazame babangu anavyokabiliwa na maangamizi kwa kiwango kikubwa kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa

**46. CAROL:** Jamani, lazima tutazame picha halisi ya tatizo hili.

**47. ALEX:** Una maana gani?

**48. CAROL:** Sio eti ni kwa manufaa yetu pekee,bali manufaa kwa watoto wetu na wajukuu wetu. Iwapo hatutachukua hatua za haraka kuyalinda mazingira yetu, basi maisha ya vizazi vijavyo yamo hatarini.

**49. CAROL:** Ni kweli kabisa! Hatuwezi kubadili uharibifu ambao tayari umefanyika, lakini tunaweza kuwapasha watu habari za uhakika na kupendekeza njia bora za kupunguza mabadiliko ya hali ya hewa

**50. LORNA:** Kweli kabisa! Unahitaji kuzunguka kote nchini ndio, lakini usitumie ndege au gari lako, au kutumia usafiri wa umma kwa mfano. Jaribu kupunguza utoaji wa gesi inayochafua mazingira.

**51. ALEX:** Nilijaribu kumueleza mkuu wa bodi ya kitaifa inayosimamia Umeme nchini, kwamba zipo njia nyingine za kuzalisha umeme pasipo kutumia machujo au mabaki ya petroli! Lakini hakutaka kujua!

**52. JOSHUA:** Bila shaka hakutaka kukusikiliza. Mifumo inayolinda mazingira sio kila mara ya rahisi au iliyo wazi. Inahitaji kufikiriwa kwa makini, muda na hata wakati mwingine masikilizano.

**53. ALEX:** **(sigh)** Sawa pia mimi munaweza kunihesabu, Ingawa najua watu wengi watanichukia..

**54. LORNA:** Kusema kweli, sidhani tutakuwa mashuhuri miongoni mwa watu wengi, lakini hilo halipaswi kutuzuia!

**END OF EPISODE THREE**

**Outro:**

Naam hadi hapo tunafika mwisho wa kipindi hiki cha Noa Bongo jenga maisha yako kwa leo.Mchezo ulioandikwa na Victoria Averill.

Ungana nasi wakati mwengine ufahamu mengi wakati kundi hili la wanafunzi linapokutana na wataalam wa mazingira ambao utabiri wao ni tisho kubwa..Na Carol ni mtu wa kwanza kupata kitisho kutoka kwa wakereketwa wa madi huu wa ujenzi wa kiwanda cha Umeme.

Na kumbuka ukitaka kukisikiliza kipindi hiki kwa mara nyingine, unaweza kutembelea mtandao wetu wa Internate d w-world.d e/ l b e

Hadi wakati huo basi kwaheri kwa sasa!